# STARDARD FOUR MID TERM 1 EXAMS-2019

## Kiswahili

*1 Hakikisha umeandika*
*(i)Jina lako* *(ii)Jina la shule yako* ***Muda: Saa 1 Dak. 40***

**Soma kifungu kifuatacho. Kina nafasi 1 mpaka 15 . Kwa kila nafasi umepewa maneno manne hapo chini. Chagua neno lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.**

Wageni walifika mle shuleni ___1___ wakawakamata watoto ___2___ waliokuwa wamepigana, wakati ___3___ kuja shuleni. Sisi ___4___ tulishtuka ___5___ kujua ___6___ kufanya. Mwalimu mkuu ___7___ ofisini akapiga simu ___8___ kituo ___9___ polisi kilicho karibu na shule ___10___. Baada ya muda ___11___ mrefu, askari ___12___ walifika wakiwa katika gari ___13___ lenye king'ora na alamu. Walitoka na bunduki ___14___ zilizokuwa na mitutu ___15___ kutisha sana.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. yetu | B. mwetu | C. petu | D. kwetu |
| **2.** | A. nne | B. mbili | C. wasaba | D. wawili |
| **3.** | A. za | B. ya | C. wa | D. la |
| **4.** | A. zote | B. sote | C. wote | D. chote |
| **5.** | A. bila | B. mbila | C. lakini | D. wala |
| **6.** | A. cha | B. vya | C. la | D. za |
| **7.** | A. alikimbizwa | B. alikimbilia | C. alikimbia | D. alikimbiza |
| **8.** | A. kwenye | B. kwenyewe | C. penyewe | D. na |
| **9.** | A. ya | B. cha | C. la | D. mwa |
| **10.** | A. letu | B. kwetu | C. yetu | D. mwetu |
| **11.** | A. isiyo | B. zisizo | C. usio | D. kisicho |
| **12.** | A. tatu | B. mbili | C. wambili | D. sita |
| **13.** | A. zao | B. yao | C. lao | D. lake |
| **14.** | A. yake | B. zao | C. lao | D. zayo |
| **15.** | A. za | B. ya | C. la | D. kwa |

**Kutoka swali 16 hadi 30, jibu kulingana na maagizo uliyopewa.**

**16. Chagua kiulizi sahihi:-**

Mwalimu anafunza somo __________?

A. mgani B. zipi

C. ngapi D. lipi

**17. Andika wingi:-**

Mtoto yule anasoma.

A. Watoto wale wanasoma.

B. Watoto hao wanasoma.

C. Matoto male manasoma.

D. Vitoto vile vinasoma.

**18. Kanusha:-**

Mtoto ameshiba.

A. Mtoto amekula.

B. Mtoto hajashiba

C. Watoto wamekula.

D. Watoto wameshiba.

19. Mgeni alikula ___________ uma na kijiko.

A. kwa B. na

C. ya D. za

**20. Kamilisha methali:-**

Usitukane _________ na uzazi ungalipo.

A. mama B. baba

C. mzazi D. wakunga

21. Ukitaka kwenda haja unasema unataka kwenda ___________.

A. jikoni B. chooni

C. kukojoa D. msalani

22. Mmea unaozaa ndizi huitwa _________.

A. mgomba B. mndizi

C. mbuni D. mpunga

**23. Kinyume:-**

Mzee huyu anacheka.

A. Mama huyu anacheka.

B. Kijana huyu analia.

C. Mzee huyu hacheki.

D. Mama huyu hacheki.

**24. Andika kwa nambari:-**

Mia sita tisini na sita.

A. 666 B. 969

C. 696 D. 6906

25. Mtoto wa mwanangu utamwita?

A. Kitoto B. Mpwa

C. Mjukuu D. Baba wa kambo

**26. Chagua sentensi iliyo sahihi:-**

A. Mtoto anavaa kusaidiwa.

B. Mtoto anafaa nguo

C. Koti lake limeumia.

D. Goti lake limeumia.

27. Ni nini maana ya msemo ***"kuaga dunia"***?

A. Kufa B. Kwenda

C. Kutembea D. Kuondoka

28. Mimea inayokua pasipotakiwa inaitwa

A. Nyasi B. Mbegu

C. Magugu D. Miche

29. Mtu asiyependa kufanya kazi huitwa

A. Mvuvi B. Maskini

C. Chotara D. Mvivu

**30. Chagua sentensi iliyo katika wakati uliopo.**

A. Nilimwona akisoma

B. Nitamwona akisoma

C. Nimemwona akisoma

D. Ninamwona akisoma

**Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali 31 - 40.**

Bidii ni mkulima mashuhuri katika kaunti. Anamiliki shamba ekari tano na ana wafanyakazi wengi. Kabla mvua haijanyesha, yeye hutayarisha shamba lake kwa upanzi. Yeye hufyeka magugu yote na mengine kuyango'oa kwa jembe. Mvua inapokaribia, Bidii na wafanyakazi wake huanza kazi ya kupanda mbegu. Mbegu huota na kuchipuka baadaye mvua ikija.

Baada ya majuma matatu hivi, huanza kazi ya kupalilia na kutoa magugu na nyasi ndogondogo. Mazao yakiwa tayari huyavuna na kuyapeleka ghalani ambapo anayahifadhi kisha bei ikipanda anayauza. Kwa hakika Bidii hupata pesa nyingi sana.

31. Bidii ni mkulima mashuhuri

A. Jijini B. Wilayani

C. Katika kaunti D. Nchini

32. Mzee Bidii hufanya nini kabla ya mvua kunyesha?

A. Hupalilia

B. Hutayarisha shamba

C. Kupanda mbegu

D. Kupalilia mimea

33. Kutayarisha shamba ni __________.

A. kuondoa magugu

B. kufyeka na kuyaondoa magugu

C. kupanda mbegu

D. kupalilia mimea

34. Bidii huanza kupalilia baada ya __________.

A. majuma mawili B. majuma manne

C. majuma matatu D. majuma matano

35. Mazao yakiwa tayari __________.

A. hupaliliwa B. hupandwa

C. huvunwa D. huuzwa

36. Chumba cha kuhifadhia mazao kinaitwa?

A. Sebule B. Ghala

C. Jukwaa D. Mekoni

37. Mzee Bidii huanza kazi ya kupanda mbegu __________.

A. mvua ikikaribia B. mvua ikipungua

C. mvua ikinyesha D. mvua ikikwisha

38. Baada ya kuvuna mazao Mzee Bidii __________.

A. huyauza B. huyapeana

C. huyapanda D. huyatupa

39. Mzee Bidii ni mkulima __________.

A. mzembe B. mwenye bidii

C. mvivu D. mlegevu

40. Hadithi hii inahusu __________.

A. Wafanyakazi

B. Kazi ya ukulima

C. Mazao ya shambani

D. Mzee Bidii

**Soma taarifa ifuatayo kisha uyajibu maswali 41 - 50.**

Mbu ni mdudu mdogo sana lakini ni hatari sana katika maisha yetu. Anapofyonza damu ya mwanadamu, huwaambukiza ugonjwa wa malaria. Ugonjwa wa malaria ni mbaya mno. Mtu akiambukizwa malaria anaweza kufa wakati wowote. Ugonjwa huu ni hatari zaidi kwa watoto wachanga.

Njia za kujikinga na malaria ni nyingi. Kwanza ni kuharibu makao yote ya mbu. Makao haya ni kama vile vichaka vilivyo karibu na nyumba zetu. Pili kufukia na kufunika mashimo yote yaliyo na maji machafu yaliyotulia. Tatu, ni kuondoa mikebe yote ambayo imekusanya maji machafu na kuitupa mbali au kuiharibu.

**41.** Mbu ni mdudu __________.

A. msafi  B. mkubwa
C. mdogo  D. mwembamba

**42.** Mbu hufanya nini damu ya mwanadamu?

A. Hunywa  B. Hufyonza
C. Huharibu  D. Hutapika

**43.** Mbu huambukiza ugonjwa upi?

A. Kifaduro  B. Malaria
C. Malale  D. Kipindupindu

**44.** Mtu akiambukizwa malaria anaweza kufanya nini wakati wowote?

A. Kuugua  B. Kutembea
C. Kupona  D. Kufariki

**45.** Ugonjwa huu ni hatari zaidi kwa akina nani?

A. Watoto wadogo  B. Wasichana
C. Wazee  D. Vijana

**46.** Njia moja ya kujikinga na ugonjwa wa malaria ni __________.

A. kujenga makao ya mbu
B. kuhamia makao ya mbu
C. kuharibu makao ya mbu
D. kukalia makao ya mbu

**47.** Ugonjwa wa malaria huenezwa sana wakati upi?

A. Kipupwe  B. Masika
C. Vuli  D. Kiangazi

**48.** Mbu hukaa sana kwenye maji __________.

A. machungu  B. machafu
C. safi  D. mengi

**49.** Tumepewa njia ngapi za kujikinga na malaria?

A. Tatu  B. Tano
C. Moja  D. Mbili

**50.** Kichwa kifaacho taarifa hii ni __________.

A. Malaria ni ugonjwa usio hatari
B. Ugonjwa wa malaria huenezwa na mbu
C. Mbung'o hueneza malaria
D. Mbu huishi kwenye maji safi

Compiled and supplied by Schools Net Kenya P.O. Box 15509-00503. Nairobi-Tel:+254202319748 |
E-Mail: infosnkenya@gmail.com | Order answers online at www.schoolsnetkenya.com